THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

# SCHOOL BASED ASSESSMENT

## KISWAHILI

## SEHEMU A

## Zoezi 1 na 2

# Gredi ya 4

## NAKALA YA MWALIMU


*© 2024 The Kenya National Examinations Council*

**Muda: Dakika 15 kwa kila mwanafunzi**

**Sehemu A inatathmini Stadi ya Kusikiliza na Kuzungumza. Inajumuisha mazoezi matatu:**

i. Mazungumzo ya ana kwa ana

ii. Ufahamu wa Kusikiliza

iii. Kusoma kwa sauti

**Maagizo ya jumla**

1. Mwalimu awafahamishe **wanafunzi wote** kwamba mazoezi yote katika sehemu hii yatakuwa tathmini ya ana kwa ana. Kila mwanafunzi atakuwa na zamu yake ya kutathminiwa; mmoja baada ya mwingine.
2. Mwalimu awafahamishe wanafunzi wote kwamba karatasi hii ina mazoezi matatu:
    i. **Mazungumzo ya ana kwa ana**
    ii. **Ufahamu wa Kusikiliza**
    iii. **Kusoma kwa Sauti**
3. Mwanafunzi aandaliwe kiti au dawati kutazamana na mwalimu.
4. Mwalimu atangulize kila zoezi na amfahamishe mwanafunzi matarajio ya kila zoezi.
5. Mwalimu amfahamishe mwanafunzi kukamilika kwa kila zoezi.
6. Mwalimu atathmini umilisi wa mwanafunzi kwa mujibu wa mwongozo wa kutathminia pamoja na kuweka rekodi.


*© 2024 The Kenya National Examinations Council*

**ZOEZI 1A: MAZUNGUMZO YA ANA KWA ANA**

**Maagizo maalum**

i. *Andaa mazingira mazuri ya tathmini kwa kumkaribisha mwanafunzi.*

ii. *Mwamkue na kumwomba akae.*

iii. *Jitambulishe kwake kwa kusema, 'Mimi ni mwalimu________________'.*

iv. *Muulize jina lake.*

v. *Anza tathmini kwa kusema,*

"Leo ningependa tuzungumze kuhusu wanyama wa porini".

1. Wanyama wa porini ni wengi. Hebu nitajie mmoja anayekuvutia.

   **(Mwanafunzi ajibu)**

2. Nieleze sababu inayokufanya uvutiwe na mnyama uliotaja.

   **(Mwanafunzi ajibu)**

3. Wanyama wa porini wasipotunzwa ni nini kitafanyika?

   **(Mwanafunzi ajibu)**

4. Badala ya kutumia neno porini tunaweza kutumia neno gani?

   (**Mwanafunzi achague kadi)**


*© 2024 The Kenya National Examinations Council*

**ZOEZI 1B: UFAHAMU WA KUSIKILIZA**

**Maagizo maalum**

*i. Msomee mwanafunzi kifungu kifuatacho* ***mara mbili.***

*ii. Mjulishe kuwa atajibu maswali baada ya kusomewa kifungu mara ya pili.*

Rona na Kadogo ni wanafunzi katika shule ya msingi ya Jitihada. Wao ni majirani. Siku moja, mwalimu wao aliwapa zoezi la kufanyia nyumbani. Rona na Kadogo waliamua kulifanya zoezi hilo pamoja.Walikubaliana kukutana nyumbani kwa kina Kadogo mwishoni mwa juma.

Rona aliwaomba wazazi wake ruhusa. Alichukua mkoba wake na kuwaaga. Rona alifika kwa kina Kadogo saa tatu asubuhi. Kadogo alimkaribisha sebuleni mwao. Walikunywa chai pamoja.

Rona alimwomba Kadogo waanze zoezi lao. Babake Kadogo, Bwana Omari, aliwapa tarakilishi yake waitumie. Kadogo alitumia nambari ya siri kuifungua tarakilishi. Walifanya zoezi hilo kwa makini. Walihakikisha kuwa wamelifanya vyema.

Bwana Omari aliwapeleka shambani. Huko walichuma mapera, maembe, maparachichi na machungwa. Kadogo na Rona waliyagawa matunda hayo katika mafungu mawili. Kadogo alimpa Rona fungu moja. Kila mmoja aliyatia matunda yake kwenye kikapu. Waliyabeba na kurudi nyumbani.

Walipomaliza kula chakula cha mchana, Rona alirudi nyumbani kwao. Alimpata mamake akitayarisha chakula cha jioni. Mamake alifurahi kumwona.

5. Rona na Kadogo wanasomea shule gani?
   **(Mwanafunzi ajibu)**

6. Unajifunza nini kutokana na kifungu hiki?
   **(Mwanafunzi ajibu)**

7. Mamake Rona alifurahi kumwona. Je, unafikiri ni kwa nini?
   **(Mwanafunzi ajibu)**

8. Kadogo alimkaribisha Rona sebuleni mwao. Je, sebuleni ni mahali gani?
   **(Mwanafunzi ajibu)**


*© 2024 The Kenya National Examinations Council*

**ZOEZI 2 : KUSOMA KWA SAUTI**

**Maagizo maalum**

i. *Mfahamishe mwanafunzi matarajio ya Zoezi la Kusoma. (Zingatia mwongozo wa kutathminia Kusoma kwa sauti).*

ii. *Mpe mwanafunzi nakala atakayoisoma kwa sauti.*

iii. *Mwanafunzi anaposoma, sikiliza na kurekodi idadi ya maneno anayosoma kwa muda wa* ***dakika moja.***

iv. *Onyesha kwa mshazari* ***(/)*** *mahali mwanafunzi alipofikia kusoma* ***dakika moja*** *ikikamilika.*

v. *Mruhusu mwanafunzi kusoma mpaka mwisho wa kifungu.*

vi. *Pigia mstari maneno* ***yote*** *ambayo mwanafunzi atashindwa kuyasoma au kuyatamka vizuri.*

vii. *Rekodi idadi ya maneno ambayo mwanafunzi ameweza* **kusoma kwa usahihi** *kwa dakika* ***moja****. (Baada ya kuondoa yaliyotamkwa vibaya au/na aliyoshindwa kutamka)*

viii. *Rekodi viwango vya umilisi wa mwanafunzi kwa kuzingatia mwongozo uliopewa.*

ix. *Hakikisha una nakala ya kurekodia tathmini hii. (Iwe na majina ya wanafunzi wote.)*

x. *Ukiwa tayari kuanza tathmini, sema,*

‘‘Sasa naomba unisomee kifungu hiki kwa sauti.’’


*© 2024 The Kenya National Examinations Council*

**Mwalimu amwambie mwanafunzi asome kifungu kifuatacho kwa sauti.**

Pendo ni afisa wa afya. Juma lililopita alikuja shuleni mwetu. [10] Alikuja kuzungumza kuhusu ugonjwa wa kipindupindu. Ugonjwa huu ulikuwa umeenea [20] kijijini mwetu.

Afisa Pendo alituambia kuwa kipindupindu ni ugonjwa unaoenea [30] kwa haraka. Alisema kwamba dalili za ugonjwa huo ni kuumwa [40] na tumbo, kuendesha na kutapika. Alituhimiza kutafuta usaidizi endapo mmoja [50] wetu angeonyesha dalili za kipindupindu.

Pendo alisema kuwa ni muhimu [60] tuzingatie usafi. Tunawe mikono baada ya kutoka msalani. Alisema pia [70] tunawe mikono kabla ya kula.// Afisa Pendo alituhimiza tuchemshe maji [80] ya kunywa. Alisema maji hayo yatiwe kwenye vyombo safi ili [90] yawe salama. [92]


*© 2024 The Kenya National Examinations Council*